**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

**SHULE YA SEKONDARI KILUVYA S.L.P 30348 DAR ES SALAAM.**

---


**MKUU WA SHULE 0785 900 146**

**MAKAMU 0718 917 95**


**MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI…………………………………..**

**S L P…………………………..**

**………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KILUVYA HALMASHAURI YA UBUNGO MKOA DAR ES SALAAM MWAKA 2023/2024**

**MAHALI SHULE ILIPO**:

Shule ya Sekondari **KILUVYA,** Ipo mkoa wa Dar es salaam, wilaya ya Ubungo Kata ya KIBAMBA mtaa wa **KILUVYA** kwa Komba.

Kutoka kituo cha daladalaMbezi Luis panda basi la kuelekea Kibaha shuka Kiluvya kwa Komba.

kutoka kibaha panda gari zinazoenda mbezi shuka kituo kiluvya kwa komba

Shule ipo umbali wa **MITA 400 kutoka barabara kuu ya morogoro**

**MUHULA WA MASOMO KWA MWAKA HUU**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya HGL /HKL /HGK kama alivyochakuliwa

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14 /8/ 2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 14/08/2023 saa 12:30 asubuhi

Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/08/2023

**MAELEZO YA SARE YA SHULE:-**

**A.WAVULANA**

- Mashati 2 meupe ya mikono mifupi yasiyobana
- Suruali mbili za rangi ya **SKYBLUE** kitambaa sample itapatikana shuleni, yenye upana wa cm 17 chini na marinda mawili kila Upande (**MARUKUFU KUBANA SURUALI-MODO) namna ya kushona imeambatanishwa**
- Soksi pair 5 rangi nyeusi
- Viatu vyeusi vya ngozi pair mbili visivyo na kisigino kirefu ( Buti au Travota haviruhusiwi)
- Vest mbili nyeupe za kiume
- Tai 2 ndefu rangi ya kitambaa cha suruali
- Nywele fupi sio kipara.
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Sare za michezo: T- shirt ( itapatikana shuleni.)
- Raba nyeupe
- sweta rangi ya maroon (linapatikana shuleni)

**B.WASICHANA**

- Mashati meupe 2 ya mikono mifupi yasiyobana
- Nusu kanzu mbili ndefu nyeupe ifike katikati ya mapaja
- Hijabu mbili nyeupe zisizo na urembo zinazofunika mikono.
- Mkanda mweusi
- Sketi pair mbili rangi ya sky blue V-shape yenye Linda la A mbele ivuke magoti. isiyobana –mshono umeambatanishwa kwa wanaovaa hijabu sketi iwe ndefu ifike kwenye kifundo cha mguu.
- Soksi pair 5 rangi nyeupe
- Viatu vyeusi vya ngozi pair mbili visivyo na kisigino kirefu.
- Nywele fupi sio kipara **(PIA UNARUHUSIWA KUSUKA NYWELE ZISIZO PUNGUA 5 NA ZISIZOZIDI 8 -MTINDO WA UTII WA RODA )**
- Vest mbili nyeupe za kike

**NB**: **Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa vitu vifuatavyo akiwa katika sare ya shule kwa mfano bangili, pete, hereni, mkufu, “bronches” soksi, viatu tofauti na sare ya shule vitu hivi vikivaliwa, vikinyang’anywa havitarudishwa.**

**C.Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni ili aweze kusajiliwa**

**Aje na Result Slip,cheti cha kuzaliwa na leaving certificate vyote vije original na nakala (MUHIMU SANA)**

i. Madaftari 07 (*counter book quire 4*);
ii. Ream **(A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. picha 2 passport size
iv. file moja
v. Madaftari madogo 7 (Msomi)
vi. Begi jeusi la kubebea vifaa vya shule
vii. Kamusi ya Kiswahili Sanifu – Oxford (**HGK**) na **(HKL)** na Dictionary ya Advance Learners kwa (**HGL**) na **(HKL)**
viii. Mathematical Set na **GRAPH PAD 2** kwa HGK na HGL .
ix. Calculator kwa wanafunzi wa **HGL** na **HGK**

**ADA NA MICHANGO YA SHULE**

***Michango inayotakiwa kulipwa na kila Mzazi/Mlezi***

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

Fedha zote hizi zilipwe kupitia akaunti ya Shule, yenye Namba **A/C 2121200114 NMB** Tawi lolote. Jina la Akaunti KILUVYA SECONDARY SCHOOL RECCURENT,baada ya malipo Bank pay slip ziwasilishwe Shuleni kwa mhasibu

***N.B:*** Mzazi/Mlezi unatakiwa kulipa kiasi cha shilingi elfu ishirini (20,000/=) kwa kila mwezi au 1000/= kila siku kwaajili ya chakula cha mchana kinachotolewa shuleni.

## D.VIFAA VYA USAFI KUJA NAVYO SHULENI

| Na. | TAHASUSI | AINA YA KIFAA |
|---|---|---|
| 1. | HGL | Fyekeo ,mkasi wa kukatia maua mmoja na ndoo ndogo moja |
| 2. | HGK | Fagio la chelewa la kusimama moja jembe moja na chepe moja. |
| 3. | HKL | Fyekeo moja ,sululu moja na fagio laini moja(soft bloom) |

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatanisho na fomu muhimu virudishwe Shuleni baada ya kujaza kikamilifu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na Fomu ya mwanafunzi kukiri kujiunga na shule .

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule CHRISTINA PATRICK MWITA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0785 900 146**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0718 917 958**
- **Mwandamizi Taaluma 0784 710 097**
- **Mwandamizi Malezi 0652 157 6767**

**KIAMBATISHO A.**

**FOMU YA KUKUBALIWA KUJIUNGA NA AHADI (1)**

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI KILUVYA

S. L. P 30348

**DAR ES SALAAM**

**KWA MWANAFUNZI**

Mimi ………………………………………………………………………………………… (Jina kamili)

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha ……… mwaka …… katika shule ya sekondari Kluvya Sekondari

**NINAAHIDI KWAMBA**

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitaweka bidii katika masomo, kazi na shughuli zote kisheria.
3. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli zote, bila kuitia hasara shule kwa kuharibu au kupoteza mali za shule.
4. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya Shule ya Sekondari Kiluvya Sekondari
5. Nitasoma kwa bidii zangu zote kuhakikisha ninafaulu na kupandisha ufaulu wa shule.

**MUNGU NISAIDIE**

**Saini ya Mwanafunzi …………………………………………..TAREHE……………………**

**KIAMBATISHO B.**

**FOMU YA KUKUBALIWA KUJIUNGA NA AHADI (2)**

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI KILUVYA

S. L. P 30348

**DAR ES SALAAM**

**KWA MZAZI / MLEZI**

Mimi (Jina la mzazi / mlezi) …………………………………………………..

Mzazi / Mlezi wa …………………………………………………………………

**NINAAHIDI KWAMBA**

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yaliyotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule pamoja
2. Nitalipa michango ya shule kwa wakati pasipo kukwamisha shughuli za uendeshaji wa shule.
3. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajiwa(Maoni, adhabu, katika kumlea mwanangu kipindi chote awapo shuleni
4. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani(Home work) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni
5. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake
6. Nitahakikisha mwanangu hafiki na simu shuleni wakati wote.
7. Nitahakikisha anahudhuria shuleni siku zote za masomo panapotokea dharura nitatoa taarifa siku ya tukio.

**JINA** ……………………………………….. **SAHIHI** ……………………………………..

**NAMBA YA SIMU**……………………………………

**KIAMBATISHO C**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

**SHULE YA SEKONDARI KILUVYA**

**YAH :<u>FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)</u>**

**SEHEMU A: IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE**

i. Jina la mwanafunzi ..........................................................................................
ii. Tarehe ya kuzaliwa .........................................................................................
iii. Uraia...................... dini.................................... dhehebu.............................
iv. Shule ya sekondari uliyosoma..........................................................................

Namba ya mtihani S. .....................................

v. Mahali unapoishi kwa sasa ..............................................................................
vi. unoishi nao kwa sasa ni wazazi /walezi……………
kama walezi uhusiano………………………..

PICHA YA MWANAFUNZI

Saini ya mwanafunzi............................................ tarehe..............................

**SEHEMU B:IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

i. Jina kamili la mzazi/ Mlezi.................................................................................
ii. Kazi ..................................................................................................................
iii. Anuani ...............................................................................................................
iv. Simu namba. 1.........................................2.......................................................
v. Sehemu unapoishi. .mtaa.............................................kata.................................

wilaya .........

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**SEHEMU C:IJAZWE NA NDUGU WA KARIBU**

vi. Jina kamili la Ndugu ........................................................................
vii. Kazi ..................................................................................................................
viii. Anuani ...............................................................................................................
ix. Simu namba. .....................................................................................................
x. Sehemu unapoishi. ..................................................mtaa................................
kata..................................................wilaya…………………

PICHA YA NDUGU

**KIAMBATISHO D.**

**UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL**
**KILUVYA SECONDARY SCHOOL**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**DATE: …………………………..**

**PART A:**
To:
Medical Officer
……………………………………………………………………………………………………………

Miss / Mr.

……………………………………………………………………………………………………………

Please examine the above named student fitness for admission:-

Put (V) for positive and a cross (x) for a negative against in a box provided

| | |
|---|---|
| Pregnancy | (  ) |
| Asthma | (  ) |
| Sight | (  ) |
| Diabetes | (  ) |
| Worm (Stool) | (  ) |
| Epilepsy | (  ) |
| TB (Tuberculosis) | (  ) |
| Sickle cell | (  ) |
| Heart disease | (  ) |
| Yellow fever | (  ) |
| U.T.I | (  ) |
| Malaria | (  ) |
| Physical disability | (  ) |

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named student and consider that he / she is physically **FIT/ UNFIT** for admission as above.

**Name: …………………………………………… Signature ……………………… Date …………………….**

**Station ………………………………………….. Destination ………………………………....**


**Official stamp ………………………………………………………….**

**KIAMBATISHO E.**

**SHULE YA SEKONDARI KILUVYA**


**MSHONO WA SKETI NA SURUALI YA MWANAFUNZI**

**MBELE** **NYUMA**




**NB:** Mshono wa sketi ni **‘‘A’’ Shape** na siyo **‘‘Solo’’ au ‘‘Tight’’ iwe ndefu isiyobana inayovuka magoti**

**MBELE**



**NYUMA**



**NB:** Mshono wa suruali usiwe ‘‘**MODO’’ Upana wa suruali chini uwe kati ya cm 17**

**KIAMBATISHO F.**

**SHULE YA SEKONDARI KILUVYA**

**ORODHA YA VITABU- KIDATO CHA TANO NA SITA**

**1. KISWAHILI**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Nadharia ya Lugha | Masebo, J. |
| ii. | Kiswahili Kidato cha 5 &6 | Oxford University Press |
| iii. | Nadharia ya Fasihi | Masebo, J. |
| iv. | Tahakiki | Masebo, J. |
| v. | Nadharia ya Lugha Kidato cha tano | Christopher Masuko, |
| vi. | Tahakiki Kidato cha Tano na Sita | Masebo, J. |
| vii. | Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita Kiswahili II 4. TIE | |
| viii. | SARUFI MAUMBO YA KISWAHILI | SAMIKISA |

**Vitabu fasihi Riwaya :**

i. Vuta ni Kuvute,

ii. Mfadhili,

iii. Usiku utakapokwisha na kufikirika.

**Tamthiliya:**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Ukingo wa Thimu, | |
| ii. | Kufikilika | Shaban Robert |
| iii. | Nguzo Mama, | |
| iv. | Kivuli kinaishi na MORANI | |

**Ushairi :**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Kimbunga, | |
| ii. | Fungate ya uhuru, | |
| iii. | Chungu Tamu na Mapenzi 5. | |
| iv. | Miundo ya Kiswahili sanifu | SAMIKISA |
| v. | Nadharia ya Lugha ya Kiswahili kilichoandikwa | P. Saluhaya |

**2. ENGLISH LANGUAGE**

| | | |
|---|---|---|
| vii. | Advanced English Language | Oxford |
| viii. | English Language | Nicholaus Ashel |

ix. Literature in English
x. Advanced Level Literature Nyambari Nyangwine 2010
xi. Advanced Level English Francis Mnyari (2014)
xii. Intoduction to Language and other books for A level Michael Kadeghe.

**Poems TIE.**

i. Selected Poems
ii. Wonderful Surgeion Charles Mloka
iii. Summorns

**Plays:**

i. I will marry when I want, Lwanda Magere,
ii. Betrayal in the city
iii. An enemy of the people

**Novel:**

i. A man of the people,
ii. A beatifuly one are not yet born
iii. His excelency the head of the state

**NB: And other A- LEVEL books.**

**3. GEOGRAPHY**

i. Physical Geography(01) D T Msabila
ii. Human Economic Geography (02) D.T Msabila
iii. Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa Longman.
iv. Kamili, 2, Physical Geography for Africa Dar es salaam Afroplus Industries.
v. Map Reading, Photography Enterpretation and Elementary Suveying D.M .Master.
vi. Research Methodology, Methods and Technique C . R Kothari
vii. Afica in Focus Physical Human and Economic Geography Revised EDITION Richard White.

**4. HISTORY**

xi. Mastering Advance Level History Book One & Two By Mwl. Kato A. Kassim
xii. Contemporary Historical Events by Comrade C. K Shibiliti
xiii. Basic themes in Advanced level History paper One by Flore M. Mavunde
xiv. Lesson Notes for Advanced Certificate of Secondary Education by Mwl. Bakari Madaya (2018)
xv. Essentials in Advanced Level History Paper 1 & 2 Saleh Yassin

**5. GENERAL STUDIES**

i. Nyambari Nyangwine, G. Bukagile and S.O. Maluka.(2010) Contemporary Approach for Advanced Level- General Studies notes form Five and Six
ii. Bigirwamungu J. and Deogratius S. M (2012) Understanding General Studies For Advanced Level Certificate
iii. Richard R.F Mbalase (2012) General Studies for Advanced Level Cetificate Afroplus Industries (T) Ltd

## <u>NB: *Ni muhimu kila mwanafunzi kuja na vitabu vya TAHASUSI anayosoma*</u>